

KCSE 2023 TOP PREDICTION MASTER CYCLE 4

KIDATO CHA NNE

KARATASI YA TATU (102/3)

MUDA: SAA 2 ½

JINA: SAHIHI:

NAMBARI YA USAJILI: MKONDO:

MAAGIZO:

- Swali la kwanza ni la lazima
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Jibu jumla ya maswali manne
- Kila swali ni alama 20
- Tumia lugha ya Kiswahili

SEHEMU YA A: USHAIRI (ALAMA 20)

Swali la lazima

Soma shairi kisha ujibu maswali

Angawa mdogo dagaa, amekomaa

Kaanga kidogo, atakufaa

Kalia kinaya, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana sio balaa

Na sio mzigo ,kijana bado wafaa

Toka kwa mtego ,kijana sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana ukubwa jaa

Jikaze kimbogo, kijana wacha kukaa

Chimbua mhogo, kijana usibung'aa

Na wake udogo, dagaa hajambaa

Kuliko vigogo ,dagaa hajambaa

Hapati kipigo ,dagaa hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa

Sihofu magego. Kijana nawe wafaa

Kazana kidogo, kijana kugagaa

Maswali

a)Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

b)Eleza arudhi zilizofuatwa katika shairi hili (alama 4)

c)Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

d)Tambua bahari katik shairi hili kwa kutegemea;

i)Vipande vya mishororo

ii)Mpangilio wa vina

iii)Idadi ya mishororo (alama 3)

e)Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 3)

f)Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 3)

g)Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

SEHEMU YA B: RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASUMPTA MATEI

2. Athari ya vita katika nchi ya Wahafidhina ni kioo cha bara ya Afrika. Jadili(alama 20)

AU

3. Riwaya ya Choji la heri imejaa aina mbalimabli za migogoro.Jadili(alama 20)

SEHEMU YA C: HADITHI YA MAPAMBAZUKO NA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

4."Ondoa wasiwasi mhibaka *you are in very safe hands* .Usiulize maswali , its okay. Tulikuja sote jana baada ya *dance* , umesahau hivi?"

i) Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)

ii) Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo.(alama 4)

iii) Jadili madhara ya pombe katika jamii kama inavyodhihirika katika hadithi ya Kila mchezea wembe. (alama 12)

Au

5. Eleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi ya Sabina.(alama 20)

SEHEMU YA YA D: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE

6. Tambua nafasi ya mwanamke jinsi alivyoshughlikiwa na mwandishi katika Tamthilia hii..(alama 20)

AU

7. 'Ulimwengu umeendelea sana'

- a) Weka dondoo katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Fafanua sifa sita za msemaji. (alama 6)
- c) Eleza kwa nini huku kwa msemaji hakujaendelea. (alama 10)

SEHEMUA YA E: FASIHI SIMULIZI

- 8.a) Taja na ufafanue hatua zozote nne za utafiti nyanjani kwa mfuatano wake. (alama 8)
- b) Tambua baadhi ya changamoto ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani (alama 8)
- c) Data iliyohifadhiwa kwa njia ya maandishi inafisha vipi uhalisia wa Fasihi simulizi? (alama 4)

Mwisho